# Idara ya Elimu

## Mwongozo wa Shule za Jimbo

## Jinsi shule za jimbo hufanya kazi

Elimu ya shule za jimbo katika jimbo la Queensland huanza na Mwaka wa Matayarisho – au Prep – na kuishia katika Mwaka wa 12. Mwaka wa Matayarisho hadi Mwaka wa 6 inajulikana kama shule ya msingi. Mwaka wa 7 hadi 12 inajulikana kama shule ya sekondari/upili.

Mwaka wa masomo huanza karibu mwishoni mwa mwezi wa Januari hadi katikati ya mwezi wa Desemba kila mwaka. Mwaka wa masomo umegawanywa katika Mihula minne, na likizo kati ya kila Muhula.

Shule ya chekechea (Kindergarten, kindy) ni mpango wa elimu usio wa siku nzima kwa watoto wa mwaka wa kabla ya kujiunga na Shule ya Matayarisho. Shule ya chekechea (Kindy) ni mahali ambapo watoto wanaweza kugundua mazingira mapya na kufurahia kusoma na marafiki. Shule ya chekechea husaidia watoto kuanza kupenda masomo na hutayarishwa ipasavyo ili kuanza shule. Ili kupata maelezo zaidi kuhusu shule ya chekechea (kindy), tembelea www.earlychildhood.qld.gov.au/early-years/kindergarten.

Watoto kutoka katika jamii maalum za jimbo la Queensland wanaweza kuhudhuria mpango wa Shule ya Chekechea Unaosimamiwa na Jimbo (SDK, State Delivered Kindergarten) katika shule ya jimbo iliyo karibu nao. Ili kujua shule ambazo zinatoa mpango wa SDK, tembelea www.earlychildhood.qld.gov.au/earlyyears/kindergarten/state-delivered-kindergarten.

Kwa maelezo zaidi kuhusu hatua za masomo, tembelea www.education.qld.gov.au/curriculum/stages-of-schooling.

## Kuchagua shule ya jimbo

Watoto wote wanaruhusiwa katika shule za jimbo la Queensland. Watoto na vijana wanaweza kujiandikisha katika shule ya jimbo iliyo karibu nao. Wazazi pia wanaweza kuchagua kuwaandikisha watoto wao katika shule maalum ikiwa wanatimiza masharti ya kujiunga.

Shule zina tovuti zao na hii ni njia bora zaidi ya kupata maelezo zaidi kuhusu shule husika. Unaweza pia kuwasiliana na shule ili kupata maelezo unayohitaji.

Kabla ya kuchagua shule, tembelea kiungo hiki kwa maelezo muhimu: www.education.qld.gov.au/parents-andcarers/enrolment/choosing-a-school

Baada ya kuchagua shule inayomfaa mtoto wako, mtoto wako atahitaji kuandikishwa katika shule hiyo. Kwa maelezo kuhusu uandikishaji, unaweza kutembelea www.education.qld.gov.au/parents-and-carers/enrolment.

Unapomwandikisha mtoto wako katika shule ya jimbo, utatoa maelezo yanayokuhusu na yanayomhusu mtoto wako. Shule za jimbo hulinda maelezo haya na haki zako za faragha kulingana na masharti ya serikali.

## Mtalaa

Wanafunzi wa shule za jimbo kuanzia Shule ya Matayarisho hadi Mwaka wa 10 hujifunza Mtalaa wa Australia (Australian Curriculum). Katika Miaka ya 11 na 12, wanafunzi wanaweza kujifunza aina nyingi za kozi na masomo makuu ambayo yanaweza kuwasaidia kupata Cheti cha Elimu cha Queensland (QCE, Queensland Certificate of Education) au Cheti cha Mafanikio ya Binafsi cha Queensland (QCIA, Queensland Certificate of Individual Achievement).

Maelezo zaidi yanapatikana katika www.education.qld.gov.au/curriculum.

Ili kupata maelezo zaidi kuhusu Mtalaa wa Australia (Australian Curriculum), tafadhali tembelea www.australiancurriculum.edu.au.
Ili kupata maelezo zaidi kuhusu QCE na QCIA, tafadhali tembelea www.qcaa.qld.edu.au.

## Kulinda wanafunzi na watoto kutokana na madhara

Katika shule za jimbo la Queensland, usalama na hali ya wanafunzi ni jambo linalozingatiwa zaidi.

Utaratibu wa ulinzi wa wanafunzi unahitaji wageni na wafanyakazi wote wa shule za jimbo kushughulikia hali yoyote inayoshukiwa ya kuleta madhara kwa mwanafunzi au mtoto na unatoa maelekezo ya wazi kuhusu jinsi ya kufanya hivyo.

Shule pia zinaweza kusaidia familia kupata huduma za usaidizi ambazo zinaweza kusaidia kukabiliana na changamoto za familia na ulezi.

Maelezo zaidi yanapatikana katika www.ppr.qed.qld.gov.au/pp/student-protection-procedure.

## Msaada wa ustawi na afya ya akili ya mwanafunzi

Shule zina jukumu muhimu katika kuendeleza ustawi wa wanafunzi na afya ya akili. Idara inatoa wafanyakazi mbalimbali wa kuwasaidia wanafunzi, ikijumuisha maafisa wa ushauri nasaha, wauguzi wa afya ya vijana wa shule, waratibu wa msaada wa vijana na wafanyakazi wengine wa msaada wa ustawi.

Idara (kupitia Zana na Nyenzo za Ustawi wa Wanafunzi (Student Wellbeing Package)) inaajiri wataalamu wa ziada wa masuala ya ustawi ili kuimarisha

huduma ya msaada wa ustawi na afya ya akili unaopatikana kwa wanafunzi katika shule zote za jimbo la Queensland. Mradi huu wa miaka mitatu wa Serikali unalenga kupanua huduma ya msaada wa ustawi na afya ya akili unaopatikana kwa wanafunzi.

## Wanafunzi kutoka asili mbalimbali za lugha na tamaduni

Kwa wanafunzi na familia za asili ya wahamiaji na wakimbizi, mashirika ya msaada wa kupata makao yanapatikana ili kutoa msaada wa kupata makao. Shule yako inaweza kukusaidia uwasiliane na mashirika haya.

Wanafunzi wote kutoka asili mbalimbali za tamaduni na lugha na familia zao wanakaribishwa katika shule za jimbo la Queensland. Misaada inatolewa kwa wanafunzi wanaoweza kuhitaji msaada wa lugha ya Kiingereza. Ili kuwa sehemu ya shule na jamii kwa ujumla. Kwa maelezo zaidi, Tafadhali tembelea www.education.qld.gov.au/students/inclusive-education/cultural-and-linguistic-diversity.

Familia zinaweza kuhitaji huduma za msaada wa mkalimani na mtafsiri. Shule yako inaweza kukutafutia mkalimani aliyehitimu, bila malipo yoyote. Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma za mkalimani na mtafsiri, tafadhali tembelea www.forgov.qld.gov.au/service-delivery-and-community-support/design-and-deliver-publicservices/interpreter-and-translator-services.

Interpreter

## Kiingereza kama lahaja au lugha ya ziada (EAL/D, English as an Additional Language or Dialect)

Kiingereza kama lahaja au lugha ya ziada (EAL/D, English as an Additional Language or Dialect) inamaanisha kwamba mwanafunzi anazungumza lugha nyingine isiyo Kiingereza na anahitaji msaada wa kujifunza lugha ya Kiingereza. Wanafunzi wa EAL/D wanaweza kujumuisha wanafunzi wa Jamii za Asili, wanafunzi wa Kisiwa cha Torres Strait au wanafunzi ambao huzungumza lugha ya Kiauslani nyumbani.

Zungumza na mwalimu mkuu wa shule yako kuhusu mahitaji ya masomo ya lugha ya Kiingereza ya mtoto wako. Maelezo zaidi yanapatikana katika www.education.qld.gov.au/students/inclusive-education/english-language-support.

## Elimu ya vipaji na talanta

Kila shule huhudumia wanafunzi wenye vipaji na talanta kwa mipango maalum ya mafunzo na masomo. Maelezo zaidi yanapatikana hapa www.education.qld.gov.au/parents-and-carers/school-information/life-atschool/gifted-and-talented-education.

## Wanafunzi wenye ulemavu

Shule zote za jimbo la Queensland hufanya marekebisho muhimu ili kusaidia wanafunzi wenye ulemavu kupata na kushiriki katika elimu kwa msingi sawa na wenzao. Marekebisho haya yanaweza kuwasaidia wanafunzi kuhudhuria shule kwa usalama, kujifunza na kufikia uwezo wao kamili.

Shule pia zinaweza kupata ushauri kutoka kwa wafanyakazi mbalimbali ikijumuisha wataalamu wa matatizo ya lugha ya matamshi, matabibu wa shughuli, wataalamu wa tibamaungo, walimu wageni wa ushauri wa matatizo ya kusikia, kuona au ya kimwili, wakufunzi wa kusoma na kuandika, msaada wa Kiauslani, na washauri wa ugonjwa wa akili wa watoto na afya ya akili. Wazazi wanaweza pia kuwasiliana na Kituo cha Ugonjwa wa Akili wa Watoto (Autism Hub) kwa maelezo na ushauri kuhusu kuwasaidia watoto wao shuleni.

Wasiliana na mwalimu mkuu wa shule yako ikiwa una maswali yoyote kuhusu jinsi shule yako inavyoweza kumsaidia mtoto wako.

Maelezo zaidi kuhusu misaada inayopatikana kwa wanafunzi wenye ulemavu yanapatikana katika www.education.qld.gov.au/students/students-with-disability.

## Wanafunzi wenye matatizo ya afya

Ikiwa mtoto wako ana tatizo la afya ambalo linahitaji kushughulikiwa wakati wa saa za shule, wasiliana na shule kuhusu jinsi ya kutimiza mahitaji ya afya ya mtoto wako, ikijumuisha kupata Huduma ya Uuguzi ya Shule za Jimbo ili kusaidia kuunda mipango na kuwapa mafunzo wafanyakazi wa shule ili wamsaidie mtoto wako kwa usalama kuhusu mahitaji yake ya msaada wa afya.

Maelezo zaidi yanapatikana katika www.education.qld.gov.au/students/student-health-safety-wellbeing.

## Kukubali wanafunzi wa kundi la LGBTIQ+

Shule za jimbo zimejitolea kutoa mazingira salama, bora na yanayokubali wanafunzi wote ambao ni wasagaji, wasenge, wanaovutiwa kimapenzi na wanaume na wanawake, waliobadili jinsia yao, wenye jinsia mbili na wasiojitambulisha na jinsia yoyote (LGBTIQ+, lesbian, gay, bisexual, transgender, intersex na queer). Shule za jimbo hushughulikia mahitaji binafsi ya wanafunzi wote ili kuhakikisha ustawi wao unakuzwa na masomo yao kuboreshwa zaidi.

Nyenzo mbalimbali zinapatikana Ili kusaidia shule, wazazi, walezi na wanafunzi kuunda na kudumisha mazingira salama, bora na yanayowakubali wanafunzi wa kundi la LGBTIQ+. Wafanyakazi wa Idara ya Elimu wanaweza pia kupata msaada kutoka kwa wafanyakazi maalum. Maelezo zaidi yanapatikana katika www.education.qld.gov.au/students/student-health-safety-wellbeing/students-with-diverseneeds#LGBTIQ+.

## Tabia ya mwanafunzi

Kwa kushirikiana na wanafunzi, wazazi na jamii kwa ujumla, wafanyakazi wetu hujitahidi kuhakikisha kila shule ya jimbo ni mazingira yasiyobagua yeyote, yanayokuza na yenye nidhamu ambapo wanafunzi wote wanaweza kujifunza, kutimiza na kufikia uwezo wao kamili.

Kila mtu hufaidika wakati shule na wazazi wanashirikiana ili kuwasaidia wanafunzi kufahamu tabia wanazotarajiwa kuwa nazo.

Wasiliana na shule ya mtoto wako na uwajulishe ikiwa una wasiwasi wowote kuhusu tabia ya mtoto wako nyumbani au shuleni. Shule itashirikiana nawe ili kutoa msaada wa mahitaji ya masomo na tabia ya mtoto wako.

Kwa maelezo zaidi kuhusu tabia za shuleni, tafadhali tembelea https://behaviour.education.qld.gov.au/ au wasiliana na mwalimu mkuu wa shule yako.

## Huduma za shirika la Queensland Health zinazotolewa katika shule za jimbo

Shirika la Queensland Health hutoa huduma za afya za bure kwa wanafunzi wa shule za jimbo, ikijumuisha uchunguzi wa macho kwa wanafunzi wa Shule ya Matayarisho, meno (afya ya kichwa) na mipango ya chanjo. Shule yako itaweza kukueleza mipango ya afya inayopatikana na wakati itakapotolewa katika shule yako. Tafadhali tembelea www.education.qld.gov.au/students/student-health-safety-wellbeing/student-health/qld-health-in-stateschools.

## Somo la dini

Somo la Dini (RI, Religious Instruction) linaweza kutolewa kwa kipindi cha hadi saa moja kila wiki wakati wa saa za shule. Somo la RI si la lazima na linaweza kupatikana kwa wanafunzi wa kuanzia Mwaka wa 1 hadi 12. Mtoto atashiriki katika somo la RI kwa kufuatia idhini iliyoandikwa kutoka kwa mzazi au mlezi wake kwa shule.

Wanafunzi ambao hawashiriki katika somo la RI hupokea somo lingine linalosimamiwa katika sehemu tofauti na mahali ambapo somo la RI linafanyika.

Maelezo zaidi kuhusu somo la RI yanaweza kupatikana kwenye tovuti ya shule yako na kwenye kiungo kilicho hapa chini.
www.education.qld.gov.au/parents-and-carers/school-information/school-operations/policy-statement.

## Spoti za Shule

Shule za jimbo la Queensland zinahimiza kushiriki, kufurahia na kukuza ujuzi kwa kuunda mipango ya spoti ambayo inatimiza mahitaji ya wanafunzi wote.

Elimu ya Afya na Mazoezi ya Mwili inatolewa kuanzia Chekechea hadi gredi ya 10 kama sehemu ya Mtaala wa Australia. Wanafunzi pia wana fursa ya kushiriki katika mashindano ya michezo kati ya shule mbalimbali na ya uwakilishaji katika kiwango cha wilaya, kanda, jimbo na kitaifa.
Maelezo zaidi yanapatikana katika www.education.qld.gov.au/parents-and-carers/activities-sports/schoolsports.

## Maafisa wa ushauri nasaha

Maafisa wa ushauri nasaha ni walimu wenye mafunzo maalum ya kusaidia wanafunzi kufaulu na kuendeleza ukuaji wao. Shule zote za jimbo la Queensland hupokea mgawo wa wakati wa ofisa wa ushauri nasaha ili kuchangia katika uundaji wa mpango wa kina wa ustawi na msaada wa mwanafunzi ambao unashughulikia mahitaji ya jamii ya shule. Msaada unaotolewa kwa wanafunzi na maofisa wa ushauri nasaha unajumuisha ushauri na nasaha kuhusu masuala ya kibinafsi, elimu, kazi, jamii, familia na ustawi na afya ya akili.

## Huduma za ukasisi na maslahi ya wanafunzi

Huduma za ukasisi na maslahi ya wanafunzi zinapatikana katika shule nyingi za jimbo na huwapa wanafunzi na jamii ya shule msaada wa kijamii na kihisia.

Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma za ukasisi na maslahi ya wanafunzi, tafadhali tembelea www.education.qld.gov.au/students/student-health-safety-wellbeing/student-support-services/chaplaincy-student-wellbeing-officer-services

## Wanafunzi wa jamii za asili na wa Kisiwa cha Torres Strait

Tunashirikiana kwa ukaribu sana na Jamii za Asili na za Kisiwa cha Torres Strait ili kusaidia vijana na elimu, mafunzo na ajira yao.

Kwa maelezo zaidi kuhusu jinsi tunavyoweza kusaidia kuboresha matokeo kwa wanafunzi wa Jamii za Asili na wanafunzi wa Kisiwa cha Torres Strait, tembelea: www.education.qld.gov.au/students/aboriginal-torres-strait-islander-education.

## Washauri wa elimu wa jamii

Washauri wa elimu wa jamii hushirikiana kwa ukaribu sana na maafisa wa ushauri na jamii za eneo lao ili kutoa msaada maalum kwa wanafunzi wa Jamii za Asili na wanafunzi wa Kisiwa cha Torres Strait.

Katika hali ambapo shule haina mshauri wa elimu wa jamii aliyeajiriwa, washauri wa elimu wa jamii wa wilaya wanapatikana ili kushirikiana na wanafunzi.

Wazazi na walezi wanaweza kuwasiliana na shule yao au ofisi ya eneo iliyo karibu kwa maelezo zaidi.

## Mradi wa Mratibu wa Msaada wa Vijana

Mradi wa Mratibu wa Msaada wa Vijana (YSCI, Youth Support Coordinator Initiative) husaidia wanafunzi wa Miaka ya 10 hadi 12 ambao wanaweza kuwa wanatatizika na elimu yao au walio katika hatari ya kuacha shule.

Mradi wa YSCI huruhusu shule maalum kuajiri Mratibu wa Msaada wa Vijana (Youth Support Coordinator) ili kutoa msaada kwa mtu binafsi, mipango ya kikundi na kutoa rufaa kwa watoa huduma wa nje kutimiza mahitaji ya wanafunzi.

## Huduma ya Muuguzi wa Afya ya Vijana ya Shule

Huduma ya Muuguzi wa Afya ya Vijana ya Shuleni (SBYHN, School-Based Youth Health Nurse) inafadhiliwa na Queensland Health ili kufanya kazi katika shule za sekondari za jimbo katika jimbo lote la Queensland. SBYHN hudumisha lengo la afya ya uzuiaji badala ya lengo la kutibu, na hufanya kazi kwa ushirikiano na shule ili kuendeleza ustawi na afya ya wanafunzi. Maelezo zaidi yanapatikana katika www.health.qld.gov.au/cq/services/school-based-youth-health-nurse.

## Mpango wa Huduma za Polisi wa Shuleni

Huduma ya Polisi ya Queensland (Queensland Police Service) na Idara ya Elimu (Department of Education) hushirikiana pamoja kuhusu Mpango wa Huduma za Polisi wa Shuleni (School-based Policing Program). Husaidia

kujenga mahusiano mazuri kati ya polisi na jamii ya shule. Maelezo zaidi yanapatikana katika www.education.qld.gov.au/students/student-health-safety-wellbeing/student-support-services/schoolbased-police-officers.

## Kushiriki kwa mzazi na mlezi

Wazazi na walezi wanaweza kuwa na jukumu muhimu katika elimu ya watoto wao. Shule za jimbo la Queensland zinathamini ushirikiano wa wazazi na walezi ili kusaidia wanafunzi katika elimu yao.

Kuna nyenzo nyingi zinazopatikana kwa wazazi na walezi ili kusaidia katika masomo ya watoto wao. Nyenzo hizi zinashughulikia umri na hatua tofauti za ukuaji. Pata maelezo kwa kutembelea www.education.qld.gov.au/parents-and-carers/community-engagement/parents.

### Kuripoti kwa wazazi na walezi

Shule hutoa hati za maelezo kuhusu maendeleo ya jumla ya mwanafunzi, mafanikio, juhudi na tabia. Shule pia zina fursa katika mwaka mzima za wazazi kukutana na walimu.

Hata hivyo, wazazi wanaweza kuwasiliana na walimu wa watoto wao wakati wowote, ili kupanga wakati wa kujadili masomo na ustawi wao.

## Kanuni za Maadili Mema ya Mzazi na Jamii

Kanuni za Maadili Mema ya Mzazi na Jamii zinaeleza matarajio 10 ya wazazi, walezi na wageni wakiwa katika mazingira ya shule ya jimbo, katika shughuli za shule na wanapotangamana na wengine katika jamii ya shule.

Kanuni hizi zimetungwa ili kujenga heshima na zinatumika pamoja na Kanuni za Maadili Mema ya Wanafunzi na Kanuni za Maadili Mema ya Huduma ya Umma ya Queensland, ambazo zinahusu wafanyakazi wote wa shule. Maelezo zaidi kuhusu kanuni hizi yanapatikana katika www.education.qld.gov.au/parents-and-carers/community-engagement/parent-andcommunity-code-of-conduct.

## Baraza za shule

Shule zingine zina baraza la shule ambalo lina jukumu maalum katika kutoa mwelekeo wa siku zijazo wa shule. Wazazi na walezi huwakilishwa kwenye kila baraza la shule na huchaguliwa kuhudumu kwa kipindi cha miaka miwili.

## Miungano ya Wazazi na Raia

Shule nyingi za jimbo zinatoa fursa kwa wazazi na walezi kujiunga katika Muungano wa Wazazi na Raia (P&C, Parents and Citizens). Miungano hii inahusika katika aina mbalimbali za shughuli za shule – ikijumuisha kuanzia kwa maduka ya shuleni, huduma ya baada ya saa za shule, kuchangisha pesa na matukio ya jamii – ili kuendeleza matokeo bora kadri iwezekanavyo kwa

wanafunzi wote. P&C ni njia nzuri kwa wazazi na walezi kuhusika katika shule ya watoto wao.

## Msaada wa Fedha

Ingawa masomo ya shule za jimbo ni ya bure kwa watoto wa raia na wakazi wa kudumu wa Australia, katika shule nyingi, utahitaji kulipia gharama ya vifaa vyako vya masomo (kalamu, vitabu, nk.) na sare za shule, kompyuta za kupakata na vifaa vingine vya kielektroniki. Shule yako itakwambia kitu ambacho mtoto wako atahitaji. Baadhi ya shughuli, kama vile kwenda kambi na ziara za masomo, hulipiwa pia na familia.

Ikiwa huna uwezo wa kulipia kitu chochote, wasiliana na mwalimu mkuu wa shule yako. Atakueleza kuhusu njia zinazopatikana.

Idara hutoa msaada wa fedha kwa familia za wanafunzi wanaohitaji msaada. Msaada unaweza kutolewa kwa ajili ya kulipia gharama tofauti, kama vile ununuzi wa vitabu vya kusoma na vifaa, usafiri wa shule na kuishi mbali na nyumbani. Serikali Kuu ya Australia (The Commonwealth Government of Australia) inaweza pia kusaidia familia kupitia Centrelink.

Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu mipango ya ufadhili ya idara kwa kutembelea tovuti zilizowekwa mwishoni mwa hati hii, au kwa kuwasiliana na mwalimu mkuu wa shule yako au Kitengo cha Msaada wa Fedha wa Shule (School Financial Resourcing Unit) kwa nambari 07 3034 5817.

## Jinsi ya kuanza

- Angalia Ramani ya Elimu (edMap) ya Idara ya Elimu ili ikusaidie kupata shule ya jimbo katika mtaa wako www.qgso.qld.gov.au/maps/edmap
- Tembelea Saraka ya Shule za Idara ya Elimu ili upate maelezo zaidi kuhusu shule za eneo lako: www.schoolsdirectory.eq.edu.au
- Wasiliana na shule na upange wakati wa kuitembelea.
- Ukiwa umechagua shule ya mtoto wako, shule hiyo itakusaidia kupitia utaratibu wa kujiandikisha.
- Ikiwa unahitaji huduma ya mkalimani, ijulishe shule na inaweza kukutafutia huduma hiyo bila malipo yoyote.

Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma zote za Idara ya Elimu zinazopatikana, tafadhali tembelea
www.education.qld.gov.au.

## Viungo muhimu

Msaada wa vitabu vya kusoma na vifaa: www.education.qld.gov.au/about-us/budgets-funding-grants/grants/parents-and-students/textbookresource-allowance

Mpango wa Msaada wa Vifaa vya Mwanafunzi:

www.ppr.qed.qld.gov.au/attachment/student-resource-scheme-srs-procedure.pdf

Msaada wa usafiri wa shule:

www.qld.gov.au/transport/public/school/school-transport-assistance/apply-for-school-transport-assistance

Msaada wa usafiri wa wanafunzi wenye ulemavu:

www.education.qld.gov.au/parents-and-carers/school-information/transport/disability-transport-assistance

au wasiliana na ofisi ya eneo ya shule yako ya jimbo:

www.education.qld.gov.au/contact-us/state-schools-regional-contacts.

Msaada wa Serikali Kuu:

www.servicesaustralia.gov.au/individuals/centrelink

Maelezo kuhusu Mpango wa Kitaifa wa Bima ya Ulemavu (NDIS, National Disability Insurance Scheme):

www.ndis.gov.au